

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

SHULE YA SEKONDARI BWERI



S.L.P 569
MUSOMA-MARA

MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI BWERI-2021

1. UTANGULIZI

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao.....

Amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **Bweri** mwaka **2021**

Tunampongeza kwa mafanikio hayo.

Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/1/2021** Na mwisho wa kuripoti ni tarehe **28/2/2021**.

Masomo yanayofundishwa shuleni hapa ni; Basic mathematics, Physics, Chemistry, Biology, History, Geography, English, Civics na Kiswahili.

2. SARE YA SHULE

- WAVULANA

Suruali rangi ya bluu bahari 2 zenye marinda mawili na upana wa kutosha, shati mikono mifupi nyeupe 2 (tomato), viatu vya ngozi vyeusi kisigino kifupi na vyenye kamba, soksi jozi 2, sweta rangi ya blue na mkanda mweusi wenye pini (usiwe utambi)

NB. Atakayekiuka maelekezo hayo hatapokelewa.

- WASICHANA

Sketi 2 rangi ya blue bahari zenye marinda-ndefu inayofunika soksi na yenye pindo lisilozidi inchi mbili na michirizi miwili (2) nyeupe chini, shati 2 nyeupe mikono mifupi (tomato), viatu vya ngozi vyeusi kisigino kifupi na vyenye kamba visiwe na urembo wowote, soksi nyeupe jozi 2, sweta rangi ya blue.

NB: Atakayekiuka maelekezo hayo hatapokelewa.

3. VIFAA VYA DARASANI.

Madaftari makubwa 9, mathematical set 1, Dictionary (english-english au english-swahili), four figure 1, kalamu za wino na penseli (vifaa vitakaguliwa kabla ya kupokelewa)

4. NGUO ZA MICHEZO

Utaribu utatolewa shuleni.

5. MAELEZO MENGINE

Muda wa kufika shuleni ni saa 12:40 asubuhi na kuondoka ni saa 11:00 jioni. Mwanafunzi mwenye ugonjwa wa kudumu aje na cheti cha daktari wa hospitali ya serikali ya mkoa (Fomu imeambatishwa nyuma.)

- **OMBI MAALUM KWA MZAZI/MLEZI:** Shule inakabiliwa na upungufu wa madawati Hivyo tunakuomba kama mzazi/mlezi ushiriki katika kumuandalia mwanao dawati kwa

kibali maalumu toka kwa mkurugenzi wa manispaa au kupitia kwa afisa mtendaji wa kata yako.

6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya mwaka **1978**. Aidha inazingatia miongozo yote

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika shughuli ndani na nje ya Shule ni muhimu.
- c) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa
- d) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hivo wakati wote uwanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya Shule.
- f) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa
- g) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote

7. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli n.k.
5. Kupigana na kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya taifa
8. Kuoja au kuolewa
9. Kupata mimba au kusababisha ndani na nje ya shule
10. Kutoa mimba
11. Kugoma/kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa Shule
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi, kuja na silaha na redio shuleni.
14. Utoro uliokithiri(siku 90 mfululizo)

Tafadhari soma kwa makini maelekezo maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu
Karibu sana katika shule yetu

Rehema D.Mwakalonge
MKUU WA SHULE.

KIAMBATISHO A

FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKUBALI MWANAE KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA

1. Mimi mzazi/mlezi(jina lako).....Mzazi/mlezi wa
.....ninaeishi Wilaya ya.....Mkoa
wa.....Nyumba na.....Mtaa.....

Nakubali mwanangu.....ajiunge na shule ya sekondari **Bweri**
kidato cha kwanza mwaka..... na kusoma masomo yote yanayofundishwa
shuleni hapo.

2. Mimi mzazi/mlezi wa kijana huyu naahidi kushirikiana na walimu katika malezi ya
mwanangu akiwa shuleni na hata nje ya shule.Na kwamba ni wajibu wangu kama
mzazi/mlezi kumhimiza mwanangu afuate sheria na taratibu zote za shule

3. Nitashiriki katika shughuli zote za maendeleo ya shule na kila mwisho wa muhula
nitamtaka mwanangu anipe taarifa ya maendeleo yake kitaaluma na kitabia

Jina la mzazi/mlezi..... Namba za simu.....

Sahihi.....

Tarehe.....

Mimi mwanafunzi.....Nimezisoma,nimezielewa na
kuzikubali taratibu na sheria za shule ya sekondari **Bweri**.Niko tayari kuzitekeleza
sheria na taratibu hizo.

Jina la mwanafunzi.....

Sahihi.....

Tarehe.....

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
(To be completed by a medical Officer in respect of form one)

Pupil's full name

Age

Blood count (red and white).....

Stool examinations

Urinalysis

Syphilis test.....

T.B test

Eye test.....

Ears

Chest

Abdomen.....

Spleen

Additional information: e.g. physical defects, infections, chronic or family diseases etc.

.....

.....

I certify that the above is fit to pursue further studies.

Signature

Designation

Station

Date